'Kuanza kwa sheria mpya za uvuvi kutaongeza uwekezaji'

Na Mwandishi Wetu, Zanzibar

KAIMU Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Emmanuel Sweke amesema kuanza kwa sheria mpya na kanuni za kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari kuu, kutaongeza uwekezaji wazawa katika bahari na kuisaidia sekta hiyo kwenda mbele.

Sweke aliyasema hayo katika mkutano wa siku moja ulioshirikisha waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali vya habari, uliofanyika Ukumbi wa Takwimu Mazizini nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Alisema sheria hiyo na kanuni zake, inalenga kuchochea uwekezaji katika uchumi wa bluu hasa kwa wazawa katika kuiendeleza sekta hiyo kwani zipo nchi nyingi, zimefanikiwa kutokana na kujiendesha kwa uvuvi na utalii.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema, ili kufikia lengo hilo katika utungaji wa sheria hiyo wametoa vivutio kwa wazawa, hasa kwa vitu ambavyo vinahitaji gharama kubwa ikiwemo vifaa vinavyoingizwa kwa ajili ya uvuvi, kupunguza ada ya leseni na vifaa vingine.

Alisema wazawa wanaweza kufaidika na uvuvi wa bahari kuu, iwapo sekta binafsi zitawekeza katika eneo hilo na kupata faida ikiwemo ajira, chakula na viwanda kukua.

"Wavuvi wetu wadogo wadogo hawana uwezo wa kuvua bahari kuu na badala yake, maji yetu yanavuliwa na meli za nje na kusababisha Tanzania kutofaidika," alisema.

Sweke alisema, Tanzania ilikuwa inapata chini ya asilimia 10 ya faida katika uvuvi wa bahari kuu hivyo kupitia sheria hiyo mapato ya nchi yanaweza kukua kutokana na uvuvi huo.

Akiwasilisha mada ya sheria na kanuni za mamlaka Ofisa Sheria kutoka mamlaka hiyo, Keis Issa Abdalla alisema sheria hiyo imezingatia mambo mbalimbali ikiwemo uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali katika ukanda wa uchumi wa Bahari ya Tanzania (EEZ).

Alisema mambo mengine ni kuongeza wigo wa mipaka ya usimamizi wa meli zenye kupeperusha bendera ya Tanzania na kuzingatia mikataba na miongozo ya kikanda na ya kimataifa ya usimamizi wa ukanda wa uchumi wa bahari na rasilimali za uvuvi zinazopatikana baharini.

Abdalla alisema, sheria kifungu cha 45 na kanuni 47 imetoa fursa kwa mwekezaji mzawa au kampuni ya Kitanzania, inayomilikiwa kwa zaidi ya hisa 51 na mzawa kuomba vivutio kupitia mamlaka.

Mbali na hayo alisema, sheria hiyo pia imetoa punguzo la ada ya leseni za wavuvi kwa wawekezaji wazawa kwa muda wa miezi sita kwa meli zenye urefu wa mita zaidi ya 50 ni dola 13,500 kwa mzawa na mgeni ni dola 545,000 sawa na upungufu wa asilimia 30, wakati meli zenye urefu wa zaidi ya mita 24 leseni ya miezi sita kwa mzawa atatoa dola 5,000 na mgeni dola 31,000, sawa na upungufu wa asilimia 16.

Alisema hatua hiyo, imefanywa kwa lengo la kutoa fursa na unafuu wawekezaji wazawa, kushiriki katika uvuvi wa Bahari Kuu.

MAJIRA UK. 16 APRIL 20, 2021

Scanned with CamScanner

Ngozi asilimia 70 inatupwa wafugaji wakibaki maskini

Na Abela Msikula

MOJA ya mazao muhimu ya wanyama wafugawao nchini kama ng'ombe, mbuzi na kondoo ukiondoa maziwa na nyama ni ngozi.

Hata hivyo, imeelezwa kwamba ni asilimia 30 tu ya ngozi ndio inayofaa kusindikwa ya nchi yetu kukadiriwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo nchini, ng'ombe takribani milioni 33.4, mbuzi milioni 21.29 na kondoo milioni 5.6.

Kiwango cha usindikaji wa ngozi nchini kinaelezwa kuwa chini ya asilimia 10, hali iliyowasukuma watafiti mbalimbali wakiwemo wa taasisi ya utafiti wa mifugo Tanzania (TALIRI) kuchunguza sababu.

Mtafiti Mwandamizi wa Taliri, Geofrey Chasama anasema katika utafiti wao imegundulika kuwa sababu moja wapo ni upotevu wa ngozi unaofikika asilimia 70 kutokana na kukosekana kwa usimamizi mzuri wa mifugo.

Inaelezwa kwamba katika machinjio upotevu wa ngozi hufikia asilimia 40 lakini malisho yasiyo sahihi husababisha upotevu wa ngozi kwa maana ya kuwa na gozi isiyofaa kwa asilimia 30.

Chasama alitoa takwimu hizo hivi karibuni katika mkutano wa uliondaliwa na Taliri na kudhaminiwa na Benki ya NMB katika Taasis ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Kampasi ya Mwanza.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya ngozi, wakiwemo wamiliki na wafanyakazi katika machinjio na maduka ya nyama pamoja na wafugaji, lengo likiwa ni kujadili uboreshaji mnyororo wa thamani katika mazao ya mifugo, hasa ngozi.

Mtafiti huyo anafafanua zaidi kwamba upotevu wa asilimia 30 hutokana na uelewa mdogo wa wafugaji katika kuhakikisha mifugo haiingii kwenye vichaka vyenye miiba inayokwaruza ngozi na kuondoa ubora wake.

Anasema ngozi ikishapata mchubuko wowote, hata ule wa kupigwa chapa sehemu isiyohusika au wanyama kupigwa fimbo mara kwa mara na kuacha alama, ngozi zao huwa batili na kutofaa tena kwa matumizi ya viwandani.

"Tunaona ni rahisi zaidi kuokoa zile asilimia 40 za machinjioni kwa ni suala la kuweka usimamizi thabiti tu, kuliko asilimia 30 za malishoni. Tunashukuru serikali imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya ngozi yaliyopelekea uwepo wa viwanda viwili vikubwa vya kusindika ngozi katika mikoa ya Morogoro na Kilimanjaro ambapo baadhi ya wataalamu wake wanaweza kushirikiana na serikali kusaidia usimamizi katika machinjio na kuhakikisha kila ngozi ya mnyama anayechinjwa inafaa kwa usindikaji," anasema.

Inaendelea Uk. 12

HABARI LEO UK-9 APRILI 20, 2021

Scanned with CamScanner

Wanawake jamii ya wafugaji walivyopunguza utegemezi

Na Mwandishi Wetu

"SIKUTEGEMEA kama siku moja ningeweza kuwa sehemu kama hii na kuwa nasimamia jengo kama hili (kiwanda). Mwaka 2015 wakati Rais John Magufuli, anazungumzia viwanda, mimi nilioni ni jambo halinuhusu," anasema na Katibu wa Jukwaa la Wakulima wadogo na wasimamizi wa masoko ya alizeti Hanan'g (JUWAMA), Andrew Jacob.

Akizungumza na waandishi wa habaria, Jacob anawashukuru wadau waliowawezesha kupata kiwanda hicho cha kuchakata alizeti kilichopo katika kijiji cha Galangala, Kata ya Lubdaw, Hanang mkoani Manyara.

Anasema wanawake na vijana walijengewa kiwanda hicho na Shirika lisilo la Kiserikali la Oxfam Hongkong kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Ujamaa Community Resource Team (UCRT), kupitia mradi wa kuwainua kiuchumi wanawake na vijana wilayani Hanang. Mbali na kujengewa kiwanda, jukwaa hilo pia limepewa zana mbalimbali kwa ajili ya zao hilo.

Zana hizo zilizoanza kutumika katika msimu wa mwaka 2019/2020, zimewezesha jukwaa hilo ambalo ni muunganiko wa vikundi sita vyenye jumla ya wanachama 174 kufungua kiwanda. Hizo ni pamoja na zana bora za kupura na kukamua mafuta ya alizeti ili kuongeza mnyororo wa thamani ili badala ya kuuza alizeti ghafi wauze mafuta ya alizeti na mashudu.

Jacob anasema awali kabla ya kujengewa kiwanda hicho walikuwa wanauza mbegu ghafi za alizeti ambazo ndizo hutoa mafuta kwa Sh 50,000 kwa gunia lakini sasa gunia hilo huwapa zaidi ya Sh 80,000 kwa mafuta na mashudu yake.

"Lakini baada ya kujadiliana na wadau wetu hao juu ya changamoto ikiwemo madalali waliokuwa wanatusababisha tupate fedha kidogo, wakaamua kutusaidia kujenga hiki kiwanda," anasema Jacob.

Anasema walipoanza kiwanda hicho baada ya kupata mashine za kupepeta, kukamua na kuchuja mafuta, wamewaweza kuepukana na madalali na hivyo kuongeza maradufu mnyororo wa thamani wa mazao yao.

Katibu huyo anasema kupitia jukwaa lao linalounganisha vikundi vya wanawake na vijana ambapo kati yao wanawake ni 158 na wanaume 16, sasa wanaweza kuchakata na kukamua mafuta ya alizeti kuanzia wanazolima wenyewe kama jukwaa pamoja na alizeti za jamii inayowazunguka.

"Kiwanda kinahudumia jamii nyingine hadi kuna wanaotoka wilaya ya Babati kuleta alizeti zao hapa ili kuzichakata. Hata katika kipindi ambacho kulikuwa na uhaba wa mafuta, sisi tuliuza sana na hatukupandisha bei zetu," anasema.

Anasema kuanzia Julai mwaka jana hadi sasa wameweza kukamua magunia 449 ya watu binafsi, nje ya jukwaa na kwamba kati ya magunia hayo, yaliyolipiwa ni 398 ambapo wamekusanya zaidi ya Sh milioni 2.3.

"Magunia mengine 46 hayajalipiwa na tuna utaratibu kwamba usipolipia unaacha mashudu ambayo kwetu yana faida zaidi kwani tunauza gunia moja kwa Sh 30,000 wakati kukamua mafuta pekee gunia moja mkulima anatulipa Sh 6,000," anafafanua.

"Kwa upande mazao yetu kama jukwaa tumeshachakata magunia 108 na kupata lita 1,710 za mafuta na tulipouza tumepata zaidi ya Sh milioni 6.47. Tulipata magunia 108 ya mashudu na kati ya hayo yamebaki 54.

"Tukiuza hayo mashudu yaliyobaki tunatarajia kupata zaidi ya shilingi milioni 1.6 na fedha zitaenda kwenye vikundi moja kwa moja kutokana na namna walivyoleta malighafi zao hapa," anasema.

Akizungumzia baadhi ya zana walizopewa, anasema kupitia trekta waliyopewa na wadau hao hadi sasa wamelima ekari 91.5 kwa gharama ya shilingi 40,000 kwa ekari ambapo hadi sasa wamekusanya zaidi ya Sh milioni 3.6.

"Ni mafanikio ambayo tumeweza kuyafikia. Kiukweli wadau hawa wameunga jitihada za serikali mkono juu ya kuhamasisha viwanda, sikuwahi kutegemea kama siku moja ningeweza kuwa sehemu kama hii na kuwa nasimamia jengo kama hili (kiwanda)," anasema.

Anasema mwaka 2017/2018 walilima ekari 42 kupitia mashamba waliyokuwa wamepewa na halmashauri na kwamba wakati wa kupalilia, watu 50 walitakiwa ili kupalilia shamba hilo kwa siku tatu kwa kutumia jembe la mkono na wakati wa kuvuna walikutana pia na changamoto kwani walikuwa wakitumia zana duni.

"Wakati wa kuvuna tulilazimika kukaa shambani kwa siku 21... Ilikuwa hatarishi kwa jamii yetu, baadhi ya wanaume waligombana na wake zao waliokuwa wameweka kambi shambani. Tulipowaeleza changamoto hiyo wakaleta mashine ya kupura alizeti.

"Msimu uliofuata halm-
shauri wali-
tupa shamba
lenye ukubwa
wa ekari 110, tu-

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti, akizungumza wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kuchakata alizeti cha jukwaa la wakulima wadogo na wasimamizi wa masoko ya alizeti (Juwama), kilichopo kijiji cha Galangala wilayani Hanang, Mkoa wa Manyara.

katumia mbegu za kisasa ambazo zinahimili ukame, ulipofika wakati wa kuvuna tulikaa shambani siku tisa, kwa sasa tunasimamia mnyororo mzima wa thamani wa zao hili wenyewe," anasema.

Anasema kimsingi kiwanda chao pamoja na zana zingine walizonazo vimewasaidia kupata kipato kikubwa kwani trekta lao wanalikodisha kwa ajili ya kubeba mazao ya wakulima wengine hadi kiwandani hapo.

Jacob anasema elimu ya matumizi ya mbegu zenye ubora na za kisasa zimewasaidia pia kuzalisha kwa wingi kwani katika gunia moja lenye kilo 70 wanaweza kupata hadi lita 33 za mafuta, huku wanaotumia mbegu za kawaida wakipata kati ya lita 12 hadi 17 tu kwa gunia.

Anasema ili jukwaa hilo liendelee na kiwanda kisife, wanajipanga ili ifike hatua ya kuachana na kulima na badala yake waingie kwenye biashara ya kununua alizeti na kuchakata mafuta pekee.

Mmoja wa wajumbe wa jukwaa hilo kutoka kikundi cha Umoja kilichopo Kijiji cha Gasaboi, Magdalena Mathias, ambaye ni mama wa watoto 10, anasema kupitia jukwaa hilo ameweza kupata mtaji wa kuanzisha biashara ya mamalishe, duka pamoja na kilimo cha mazao mengine.

Anasema awali kabla ya elimu kutolewa na Ujamaa Community Resource Team (UCRT) katika maeneo hayo ya vijijini wanawake walikuwa hawafanyi biashara na badala yake walikuwa wakitegema waume zao tu.

Anasema amekopa mara kadhaa ikiwa ni pamoja na kuongezea kwenye ujenzi wa nyumba yake ya kisasa.

"Nilikopa Sh 500,000 na kabla ya hapo nilichukua Sh 100,000 na kuanza biashara ya mgahawa. Bila UCRT na wadau wengine wa maendeleo maisha yangebaki kuwa ya shida kama zamani. Nisingeweza kupeleka watoto shule. Kwa kweli wametusaidia kwani tumeondokana na maisha duni na sasa hivi hatuogopi kusomesha watoto hata mwanaume akikataa naweza kusomesha watoto mwenyewe," anasema kwa kujiamini.

Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Martha Suley, anashukuru kwa elimu ya ujasiriamali waliopata kwani imewasaidia kwa kiwango kikubwa kwa vile awali katika jamii hiyo ya wafugaji wanawake walibaki kuwa watu wa kuwategemea waume zao tu.

Anasema baada ya elimu hiyo akina mama wameanza kujitegemea na kukopa kupitia vikundi vyao na faida wanayopata wanaitumia kwa ajili ya miradi mingine.

"Kwa desturi ya kwetu mwanaume ndiye alikuwa anamiliki kila kitu, hata kama wakati unaolewa ulipewa mifugo, inakuwa mali ya mume. Baada ya mafunzo mimi binafsi nimenufaika kwa sababu nimekuwa na shamba langu tofauti na la familia. Nilikopa pesa ya kikundi nikakodi shamba na kulima mahindi na maharage.

"Uwepo wa kiwanda hiki hapa kijijini, wananchi wenzetu wanatupongeza kwani ni hatua kubwa. Julai mwaka jana nilikopa Sh 200,000, nikanunua nguruwe watatu kila mmoja Sh 50,000 na Sh 50,000 iliyobaki nikanunulia mashudu.

"Niliwalisha na kuwanenepesha na mwezi Desemba niliwauza Sh150,000 kila mmoja. Fedha niliyopata niliitumia kulima shamba la familia lenye ukubwa wa ekari nne na tunatarajia kupata gunia 60," anasema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilaya ya Hanan'g, Dorris Ng'homange, anasema mchango wa wadau katika wilaya hiyo unasaidia wananchi kukua kiuchumi huku wanawake wakianza kumiliki uchumi na taratibu kuondokana na mfumo dume.

Anasema kupitia wadau hao wananchi wamefaidika na mradi wa mpango wa matumizi bora ya ardhi uliowezesha wanawake kumiliki ardhi kwa hati jambo ambalo kwenye wilaya hiyo halijawahi kutokea.

"Tumekuwa na mabaraza ya kimila ni mchango ambao tunauthamini sana, hasa ikizingatiwa eneo hili ni wilaya ya wafugaji, mfumo dume unatawala. Awali unyanyasaji wa kijinsia ulikuwa ni mkubwa lakini kupitia mabaraza ya kimila yamesaidia kuna mabadiliko makubwa wanawake wanajitambua.

"Kupitia wadau hao tumenufaika na mradi wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, wanawake wamefanikiwa kumiliki ardhi kwa hati, jambo ambalo kwenye wilaya yetu halijawahi kutokea na hali ya uchumi imeimarika," anasema na kuongeza kwamba wakati mwingine udhalilishaji wa kijinsia au ukatili kutokana na akina mama kutokuwa na kitu.

Afisa huyo anaomba wadau wengine wa maendeleo kuendelea kushirikiana na serikali ili kusaidia jamii ikue kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Msajili wa taasisi zisizo za kiserikali (NGOs) ambaye pia ni mratibu wa viwanda wilayani humo, Gaudance William anasema Juwama ni miongoni mwa viwanda muhimu wilayani humo kinachoweza kuchakata zaidi ya tani tatu za mafuta ya alizeti kwa siku.

"Kiwanda kina ufanisi mkubwa hivyo nitoe wito kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika halamashauri yetu waje, fursa ni nyingi na mazao mengi yanazalishwa hapa kwani tumekuwa tukipata changamoto ya uongezaji thamani mazao," anasema.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti, akikabidhi trekta kwa kiwanda cha kuchakata alizeti kwa jukwaa la wakulima wadogo na wasimamizi wa masoko ya alizeti Hanang (Juwama) lililotolewa na Shirika lisilo la Kiserikali la Oxfam Hongkong. (Picha zote na Mpigapicha Wetu).

MAJIRA.

TMDA yabaini dawa bandia ya mifugo

Uk. 4

Scanned with CamScanner

na mitandao mmoja wa kijamii.

TMDA yabaini dawa bandia ya mifugo

Na Penina Malundo

■■MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imebaini uwepo wa dawa bandia ya mifugo aina ya Alben Blue 2.5% toleo Na.019394 lililotengezwa Nov 2019 na yenye tarehe ya mwisho wa matumizi Oktoba 2022 katika soko .

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo alisema mamlaka hiyo kupitia mifumo yake ya ukaguzi na ufuatiliaji wa bidhaa katika soko iliweza kufatilia na kugundua uwepo wa dawa hiyo bandia.

Alisema dawa hiyo katika lebo yake inaonesha inatengenezwa na kiwanda cha Nerix Pharma kwa niaba ya Vetagro and Pulper Co.Ltd Nairobi nchini Kenya.

Alisema kuwa katika kufanya uchunguzi wa kimaabara ambapo matokeo ya uchunguzi yameonesha kuwa toleo hilo halina kiambata hai.

"Wafanyakazi wote waliokutwa na toleo hili wamefunguliwa mashitaka katika vituo mbalimbali vya polisi na upelezi unaendelea ili kuweza kuutambua mtandao mzima unaojihusisha na utengenezaji ,usambazaji na uuzaji wa toleo hilo bandia la dawa hii," alisema.

Alisema kutokana na kubainika dawa hiyo, wafugaji wote nchini wanaotumia dawa hiyo kwa ajili ya kuua minyoo wanaelekezwa kuangalia kwa makini lebo za dawa hiyo na endapo wataona namba za toleo husika watoe taarifa katika Ofisi zao.

"TMDA inaendelea kuwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa ikiwa watabaini kampuni, kikundi, mitandaoau mtu yeyeto anayejihusisha na utengenezaji usambazajiau uuzaji wa dawa hii ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi yao," alisema.

Scanned with CamScanner